HALMASHAURI YA WILAYA YA HANDENI
SHULE YA SEKONDARI KWAMKONO
S.L.P. 262,
HANDENI – TANGA.
SIMU: 0659985018

Kumb. Na. **KMSS/A1/S951/43/20** TAREHE: **14 December 2020**

MZAZI/MLEZI WA: .....
.....
.....

YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA KWANZA MWAKA 2021

1.0. UTANGULIZI.

Ninafuraha kukuarifu kuwa mwanao mtajwa hapo juu amechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika shule hii mwaka 2021, HONGERA SANA.
Shule ya Sekondari Kwamkono ipo katikati ya Vijiji vya Mbuyuni na Kwamkono ikiwa ni mita 100 Kaskazini mwa Hospitali ya St. Francis Kwamkono.

1.1. Shule ya Sekondari Kwamkono itafunguliwa rasmi tarehe **11.01.2021** Mwanao anatakiwa kuripoti shuleni siku hiyo **saa 1.00 asubuhi** bila kukosa. Siku zinazofuata za maisha ya uanafunzi wake anatakiwa kuripoti **saa 12:30 asubuhi** bila kukosa. Mwisho wa kuripoti kwa hiari ni tarehe **18.01.2021** baada ya hapo HATUA KALI ZA KISHERIA zitachukuliwa dhidi ya Mzazi/Mlezi atakayeshindwa kumleta mwanae shule.

Mafunzo ya awali ya Kiingereza (**English Orientation Course**) yataanza mara moja baada ya kuripoti shuleni. Na nivizuri kumleta mwanao wewe mwenyewe mapema iwezekanavyo ili awe na mtiririko mzuri.

1.2. Shule hii ni ya kutwa (Day School) na hostel kwa wasichana hivyo utahiari mwanao kulala nyumbani na kuja shuleni kila siku asubuhi saa 12:30 na kurudi nyumbani saa 11:30 jioni kama ratiba ya shule itakavyoelekeza au kumleta hostel kwa masharti utakayopewa na shule. Kama utampangishia mwanao chumba hakikisha unaweka uangalizi wa karibu ili kuhakikisha kuwa mwanao anafika shule ipasavyo kwani kuna watoto wengi hawajitambui na kuishia kulala kwenye vyumba vyao na kuwa watoro wa masomo shuleni.

2.0. MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA.

2.1. SALE ZA SHULE.

(a) **Wavulana:-** - Suruali mbili za rangi ya damu ya mzee yenye marinda mbele.
- Soksi nyeusi.
- Shati jeupe la mikono mifupi (kubwa linalomtosha kwa umbile lake).

(b) **Wasichana:-** - Sketi ndefu mbili zinazofikia kwenye kungu mbili za miguu za rangi ya damu ya mzee yenye marinda ya kawaida yasiozidi 14.(sketi (sketi isiyokidhi vigezo haitokubalika)
- Soksi ndefu nyeupe (Stockings).
- Shati jeupe la mikono mifupi (kubwa linalomtosha kwa umbile lake).

(c) **Hijabu kwa wanafunzi wa kike wa Kiislam.(KIAMBATANISHO A)**

Kila mwanafunzi wa Kiislam aliyekuwa tayari kwa vazi hilo anatakiwa:-

- Sketi ndefu pana inayofikia katika kungu mbili za miguu.
- Nusu kanzu ndefu na pana inayotosha mwili wake (ifike mapajani)
- Scalf (juba) jeupe refu litakalomfunika kuanzia kichwani hadi katikati ya mapaja na magoti.

Kila mwanafunzi awe na sare mbili zilizokamilika. Ni vema kila mzazi mwenye binti wa kiislam amshonee mwanae vazi hilo kwani hatutamruhusu mwanafunzi kuja shuleni na mitandio ya namna tofauti katika kipindi cha dini.

TANBIHI.

Kila mzazi amshonee mwanae nguo za shule kulingana na maelekezo haya na si vinginevyo. Mwanafunzi atakayeletwa akiwa na suruali inayobana (Modo) au sketi fupi na shati zinazobana atapewa adhabu kali ikiwa ni pamoja na kusimamishwa shule. **Shati/Juba ni lazima liwe na nembo ya shule ambayo itapatikana hapa shuleni.**

(d) **Sare ya kazi.**

Kila mwanafunzi lazima awe na sare ya kazi ambayo itavaliwa siku za kazi au baada ya darasani ambayo itakuwa ni **Suruali/Sketi nyeusi** na **fulana ya shule (T.Shirt)** na viatu vya kudumbukiza rangi yoyote.

(e) **Cheti cha kuzaliwa.**

Kila mwanafunzi aje na kivuli cha cheti cha kuzaliwa.NI MUHIMU iwapo hujui utaratibu wa kupata cheti cha kuzaliwa fika shuleni kwa USHAURI.

2.1. VIFAA VYA DARASANI.

Kila mwanafunzi atasoma masomo tisa (09) ya **lazima** na moja la ziada kwa wanafunzi wa Kiislamu. Hivyo ni bora kila mzazi amnunulie mwanae vitu vifuatavyo:-

- Daftari au counter books (2 Quire) 10 za nukuu za masomo na daftari 10 za mazoezi.
- Kalamu za kutosha (nyeusi na bluu tu).
- Mkebe na vifaa vyake, **rula, penseli** na **Kifutio** ni lazima.
- Begi imara la kubebea daftari, kamwe daftari na vitabu visibebwe mikononi.

2.2. HUDUMA ZA AFYA.

Kila Mzazi/Mlezi atalazimika kumhudumia mwanae mara tu atakapougua kwani shule haina Zahanati au huduma yoyote ya afya. Wazazi wenye watoto wa kike wenye matatizo ya mashetani watibiwe ipasavyo kwani kuna wimbi la wazazi lililozuka hivi karibuni kuwa mwanaye anatakiwa asinyoe nywele kitu ambacho kipo kinyume na sheria za shule.

2.3. VIFAA VYA USAFI.

Kila mwanafunzi anatakiwa awe na vifaa vya kufanyia usafi na shughuli za miradi shuleni. Hivyo basi atalazimika kuwa na **Fagio kubwa la chelewa , Jembe ,Kwanja na kindoo.**Kila mwanafunzi atawajibika kuvitunza vifaa hivyo mahala atakapoishi ili vitakapohitajika kwaajili ya ukaguzi/kazi atavileta na vyote vitabaki kuwa Mali yake.

3.0. LUGHA YA MAWASILIANO.

Lugha ya mawasiliano shuleni hapa ni KIINGEREZA na KISWAHILI TU. **Masomo yote yanafundishwa kwa lugha ya kiingereza** isipokuwa somo la Kiswahili na Elimu ya dini ya Kiislam. Hivyo mhimize mwanao akija

hapa ajifunze kwa bidii kuzungumza na kuandika vizuri kiingereza ili aweze kumudu masomo yake vizuri zaidi. Aidha mzazi unashauriwa kumnunulia mwanao Kamusi (dictionary) ya **ENGLISH – KISWAHILI** ili imsaidie kutafsiri maneno magumu ya Kiingereza yatakayomshinda kwa kuwa shule haina kamusi hizo.

4.0. RIPOTI YA MAENDELEO.

Kila shule inapofungwa mwisho wa mhula (**June na Disemba**) hakikisha unafika shuleni kuchukuwa ripoti ya maendeleo yake kama utakavyotaarifiwa na uisome kwa umakini ili uweze kusaidiana na walimu kumshauri mwanao.

4.1. UTORO.

Wanafunzi wengi wamekuwa watoro sana wa shule kwa **kukosa uangalizi wa karibu** hasa pale wanapokuwa wanaishi katika nyumba za kupanga au hata kwa ndugu au nyumbani kwao.

Tunakuomba sana mzazi uhakikishe unamsimamia mwanao ipasavyo ili kuhakikisha kuwa anajitambua na anatambua wajibu wake wa kuwa yeye ni mwanafunzi na anatakiwa kufika shule kila siku na **kuhudhuria vipindi vyote** bila kukosa. Aidha kama kuna tatizo la kijamii **mzazi/mlezi ndiye pekee tutakayekutambua katika kutoa taarifa ya kutofika kwa mwanao shuleni**. Mzazi/Mlezi usimuache mwanao afanye atakavyo kwa kuwa Elimu ni bila malipo, kufanya hivyo ni makosa, hivyo kila mmoja awajibike kwa nafasi yake. **Iwapo mzazi utapata taarifa ya kuhitajika shuleni,fika mara moja kwa ustawi wa mwanao na shule kwa ujumla.** Aidha **wazazi wanaowapangishia watoto wao wahakikishe kuwa wanawapa huduma stahiki ili kuepusha utoro wa rejareja na kutomudu masomo kwa kukosa mahitaji**

4.2. SHERIA ZA SHULE.

Kila Mzazi/Mlezi na mwanafunzi wanapaswa kuzisoma sheria za shule zilizoambatanishwa ili mzazi umshauri mwanao kuhusu maisha yake awapo shuleni.

4.3. HUDUMA YA HOSTEL.

Shule ina hostel ya wasichana, hivyo kama mzazi atahitaji mwanae kuishi Hostel, fika shuleni ili upate utaratibu.Nafasi ni chache hivyo ukipewa taratibu zote zitimize kwa wakati.

4.4. FOMU MUHIMU ZA KUJAZA.

Fomu zifuatazo ni **lazima zirudishwe shuleni** zikiwa zimejazwa kikamilifu siku ya kuripoti shuleni:-

- Fomu ya vipimo vya kiafya (Medical Examination Form) ijazwe na Daktari na agonge mhuri wake.
- Fomu ya kiapo cha utii ya mwanafunzi awapo shuleni na mkataba wa mzazi na shule.

4.5. MWISHO.

Kwa niaba ya watumishi wote wa Shule ya Sekondari Kwamkono, ninamkaribisha mwanao hapa shuleni kwa kumtakia mafanikio mema kipindi chote cha maisha yake shuleni. Ninamshauri mwanao awe na **malengo** yatakayo mfanya awe na bidii ya masomo awapo shuleni na **aepuke** makundi maovu ili aweze kufikia malengo yake kwa manufaa yake /Familia/Jamii na Taifa kwa ujumla.

KARIBU SANA KWAMKONO SEKONDARI.

Nongwa

(SHAWEJI H. NONGWA)
MKUU WA SHULE
Headmaster
3
Kwamkono Secondary School
P. O. Box 262 Handeni



KIAMBATANISHO A

HANDENI DISTRICT COUNCIL
KWAMKONO SECONDARY SCHOOL
P.O.BOX 262,
HANDENI – TANGA.
MEDICAL CERTIFICATE FORM

To be completed by Medical Officer in respect of form I/V.

(i) Pupil's name: .....
(ii) Age: .....
(iii) Blood count (Red and White): .....
(iv) Stool: .....
(v) Analysis: .....
(vi) Syphilis test: .....
(vii) T.B. Test: .....
(viii) Ears: .....
(ix) Chest: .....
(x) Spleen: .....
(xi) Abdomen: .....

ADDITIONAL INFORMATION: E.g. Physical defects or Impairments, Infection, Chronic or family diseases etc.

.....
.....
.....
.....
.....
.....

I certify the above is fit/unfit for admission into a secondary school.
Designation: .....
Station: .....
Date: .....
Official stamp:

HATI YA KIAPO CHA UTII

Mimi (Mwanafunzi _____ ninakiri kuwa nimesoma maelekezo yote na NINAAHIDI kuwa SITOFANYA KOSA lolote litakalofanya mimi nirudishwe nyumbani NINAAHIDI kushirikiana na Wanafunzi wenzangu, Viranja, Walimu na Watumishi wengine kwa mafanikio yangu.

NINAAHIDI kuwa sitogomea adhabu, na wala sitachochea, kushiriki au kuongoza mgomo niwapo shuleni.

_____ _____ _____

(Sahihi ya mwanafunzi) (Tarehe) (Sahihi ya Mzazi- Shahidi)

MKATABA WA MZAZI NA SHULE.

Mimi Mzazi/Mlezi wa mwanafunzi _____ ambaye jina langu ni _____ nimesoma maelekezo haya kwa makini na ninakubaliana/sikubaliani nayo kutumiza masharti yote yaliyopo ndani ya barua hii na ninaahidi USHIRIKIANO MKUBWA.

_____ _____ _____

(Sahihi ya Mzazi/Mlezi) (Tarehe) (Sahihi ya shahidi – Mwanafunzi)

_____

(Namba za simu za Mzazi/Mlezi)

*Kata isiyohusika

SHERIA NA KANUNI ZA SHULE.

Wanafunzi wote wanapaswa kuzingatia na kufuata sheria na kanuni za shule kama ifuatavyo:-

1. Kila mwanafunzi anatakiwa ajiheshimu mwenyewe, wanafunzi wenzake, walimu, watumishi wengine wa shule na watu wengine na anatakiwa kusimama apitapo mwalimu au mtu aliyemzidi umri.

2. Kila mwanafunzi anatakiwa kushiriki, kuheshimu na kuthamini kazi za mikono na aelewe kuwa ni sehemu ya maisha yake.

3. Kila mwanafunzi anatakiwa kuwahi shuleni kila siku saa 12:30 asubuhi au kabla na kutii wito wa kengele kwa kukimbia na anatakiwa aondoke shulenii saa 11:30 jioni kwa ruhusa ya mwalimu wa zamu kila siku.

4. Ni lazima kila mwanafunzi ahudhurie vipindi vyote vya masomo ndani na nje ya darasa na ashiriki kikamilifu katika kazi zote atakazopewa na kwa uadilifu. Mwanafunzi yeyote atakayekiuka atapewa adhabu kali.

5. Kila mwanafunzi anatakiwa kuheshimu Bendera ya Taifa, Wimbo wa Taifa, Fedha za Taifa na Nembo ya Taifa.

6. Kila mwanafunzi anawajibu wa kuzilinda na kuzitunza mali za shule, zake binafsi na za wanafunzi wenzake.

7. **Ni marufuku kabisa:-**
   - (i) Kutumia lugha ya matusi au kejeli shuleni.
   - (ii) Kunyoa nywele fasheni kama vile upara, Kiduku, Panki, Kisahani n.k ni wajibu wa kila mwanafunzi kunyoa nywele zake kawaida (zinazolingana kichwa chote). Ni marufuku kusuka nywele kwa wasichana.
   - (iii) Kupiga kelele darasani au katika mikutano na mikusanyiko mingine.
   - (iv) Kufuga kucha, ndevu, kuweka rangi kwenye kucha, nyusi midomo na n.k. Mwanafunzi yoyote atakayeonekana kujipendezesha kwa rangi au vipodozi atapewa adhabu kali.
   - (v) Kujichubua kwa mikorogo ya namna yoyote ile. Ikibainika unatumia dawa ya kujichubua utarudishwa nyumbani hadi hapo ngozi yako itakapokuwa kama ya asili.
   - (vi) Kuwa mchafu wa mwili na mavazi.
   - (vii) Kutoka nje ya shule bila ruhusa kutoka kwa mwalimu wa zamu.
   - (viii) Kutembelea maeneo ya starehe kama baa, vilabu vya pombe, nyumba za wageni na kumbi mbalimbali za starehe.
   - (ix) Kuingia maabara na ofisini bila ruhusa ya walimu.
   - (x) Kuvuta sigara, bangi, kunywa pombe au matumizi yoyote ya madawa ya kulevya.
   - (xi) Kutovaa sare za shule, uvaaji wa viatu visivyotakiwa kama bajaji, ndala, kata mbuga, yeboyebo n.k. au kuvaa shati lisilo na nembo ya shule.

8. Mwanafunzi atafukuzwa shule kwa makosa yafuatayo:-
   - (i) Uasherati, ubakaji na ushoga.
   - (ii) Wizi.
   - (iii) Uvutaji bangi na vilevi vya aina zote.
   - (iv) Kupigana au kupiga au kutishia kupiga.
   - (v) Kuharibu kwa makusudi mali za shule au ya umma.
   - (vi) Kuoa au kuolewa.
   - (vii) Kupata mimba au kuharibu na kutoa mimba.
   - (viii) Kusababisha mimba nje na ndani ya shule.
   - (ix) Kugomea adhabu.
   - (x) Kugoma, kuchochea au kuongoza mgomo unaoweza kuvuruga amani ya watu.
   - (xi) Kutohudhuria shule kwa muda mrefu bila sababu ya msingi.
   - (xii) Kuwa na simu ya mononi.

9. Ni wajibu wa kila mwanafunzi kutii amri ya kiranja, walimu na wafanyakazi wasio walimu. Iwapo mwanafunzi ataonesha dalili ya dharau hatua za kinidhamu zitachukuliwa dhidi yake.

10. Kila mwanafunzi anapaswa kufahamu kuwa sheria za shule ni kwaajili ya kumlinda na kumuongoza ili aweze kunufaika na uwepo wake hapa shuleni. Hivyo basi kila mwanafunzi anatakiwa kuweka mbele utii na nidhamu na ndipo atakapopata Taaluma ipasavyo na hatimae kufanikiwa.